# HALMSHAURI YA WILAYA YA UYUI

**Tarehe 26 Julai 2025**, Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui umbali wa Kilometa **190.64.** Jumla ya miradi sita **(06)** ya maendeleo yenye thamani ya shilingi **1,467,821,700.00** itakaguliwa, itazinduliwa, itatembelewa na Kuwekwa Mawe ya msingi. Miradi hiyo inatoka katika sekta za Elimu, Afya, Maji, Barabara, Maendeleo ya Jamii, na Maliasili.

Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;

i. Mradi wa useremala wa vijana unaotengeneza bidhaa za Mbao Tura kutokana na Mikopo ya asilimia Kumi – **Mwenge utatembelea Mradi**.

ii. Mradi wa Mabweni mawili ya wasichana Shule ya sekondari Tura – **Mwenge utazindua Mradi**.

iii. Mradi wa kituo cha kukusanya,kuchakata na kuuza asali kilichopo katika Kijiji cha Tura - **Mwenge utaweka Jiwe la msingi**.

iv. Mradi wa barabara kwa kiwango cha udongo na changalawe chenye urefu wa kilometa **14.5** Kizengi hadi Gengesita - **Mwenge utatembelea Mradi**.

v. Mradi wa jengo la upasuaji la (Mama na Mtoto) la kituo cha Afya kizengi - **Mwenge utatembelea Mradi**.

vi. Mradi wa Uchimbaji na uendelezaji wa visima kumi **(10)** wilaya ya Uyui Kijiji cha Mpumbuli katika kata ya kizengi – **Mwenge utaweka Jiwe la Msingi.**

Aidha mapokezi ya **Mwenge wa Uhuru 2025** yatafanyika kwenye uwanja wa Michezo Shule ya sekondari Tura na baadaye Mkesha utafanyika Stendi ya Kigwa siku ya Jumamosi **Tarehe 26 Julai 2025**.

***"Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu Mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu"***

## 'WANANCHI WOTE MNAKARIBISHWA'